

LAIKIPIA



UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2ND SEMESTER 2023/2024 ACADEMIC YEAR

SECOND YEAR EXAMINATIONS FOR BACHELOR OF ARTS KISWAHILI AND COMMUNICATION

KICO 221: FASIHI SIMULIZI NA MAWASILIANO

STREAM: R

TIME: 2 HRS

DAY: WEDNESDAY (11.30-1.30PM)

DATE: 17/4/24

THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF TWO (2 PAGES)

PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.



MAAGIZO: Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine yoyote **MAWILI**

SWALI LA KWANZA (ALAMA 30)

- a) Onyesha nafasi ya mandhari katika kuwasilisha ujumbe kwa utanzu wa maigizo. **(Alama 8)**
- b) Kuna umuhimu anuai wa mwanafunzi wa Kiswahili na Mawasiliano kusomea kozi ya fasihi simulizi. Huku ukitolea mifano mwafaka jadili ukweli wa kauli hii. **(Alama 10)**
- c) Taja na ueleze kwa kifupi hatua zote zinazozingatiwa kwenye mchakato wa ukusanyaji wa data za fasihi simulizi nyanjani. **(Alama 12)**

SWALI LA PILI (ALAMA 20)

Kwa kila mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vifuatavyo vya semi, ainisha muundo, Sifa na umuhimu wake: **(Alama 20)**

- i. Nahau.
- ii. Vitendawili.
- iii. Methali.
- iv. Vitanza ndimi.

SWALI LA TATU (ALAMA 20)

- a) Thibitisha namna fasihi andishi ilivyo na msingi wake katika Fasihi Simulizi ya Kiswahili. **(Alama 08)**
- b) Kadiria uzito na udhaifu wa mbinu zozote *NNE* za kukusanya data nyanjani katika fasihi simulizi na mawasiliano. **(Alama 12)**

SWALI LA NNE (ALAMA 20)

- a) Bainisha changamoto zinazojitokeza kwenye mchakato wa kukusanya data za fasihi simulizi nyanjani. **(Alama 08)**
- b) Jadili namna fani inavyochangia pakubwa katika ubainisha wa maudhui katika vipengele vya Fasihi Simulizi; **(Alama 12)**

SWALI LA TANO (ALAMA 20)

- a) Kijielezi cha maana ya fasihi kimebeba vipengele vinavyobainisha nafasi ya fasihi. Jadili ukweli wa usemi huu simulizi katika mawasiliano. Thibitisha. **(Alama 08)**
- b) Fasihi simulizi ina nafasi nzuri kuchangia utatuzi wa baadhi ya changamoto za kijamii. Jadili. **(Alama 12)**

